






Wekesa alikuwa na donda
mguuni. Yeye na mkewe
waliishi kijijini na wanao.



Binti yao, Nangila, na kaka
zake watatu walifanya kazi
zao vizuri.




Nangila aliwavutia wengi.
Mwanamme aliyependa
kumwoa, alitakiwa kutimiza
sharti kali lililowekwa na
babake.




Sharti lilikuwa kuileta miti-shamba kutoka ziwa lililokuwa karibu. Dawa hiyo ingeponya donda alilokuwa nalo bababke Nangila. Ziwa hilo lilijaa mizimu hatari.




Baadhi ya wanaume waliojaribu kuipata ile miti-shamba, walirudi mikono mitupu. Wengine kamwe hawakurejea kutoka ziwani.




Nangila alikuwa na hofu
kaka zake pia
waliposhindwa kwenda
ziwani. Aliamua kwenda
mwenyewe. Mamake
alimwambia, "Mwanangu,
wanaume wameshindwa,
utafaulu?"



Nangila alimsaidia bi kizee
mmoja kubeba kuni. Bi kizee
alimshukuru, akamwambia,
"Nitakueleza jinsi
utakavyofika kwenye ziwa la
mizimu na namna
utakavyofanya."




Nangila alipofika kwenye ukuu wa ziwa, alionna familia ya mizimu ikinywa na kushereheke. Alisubiri na kutazama. Moja baada ya nyingine, mizimu ilipatwa na usingizi.




Mizimu yote ilipolala,
Nangila alipiga mbizi
ziwani. Aliipata miti-shamba
na kuiweka mkobani.
Alipoogelea kurudi ufuoni,
mawimbi makubwa
yalimzunguka.



Alifika ufuoni mizimu ikiwa
imeamka. Aliimba wimbo
aliofunzwa na bi kizee: Mie
nilikuja kwa sababu
wanaume waliogopa.
Babangu ahitaji dawa. Ndiyo
sababu nikaja hapa.



Sauti ya Nangila ilikuwa
tamu sana hata mizimu
ikamtaka aendelee kuimba.
Mizimu ilipolala tena,
Nangila alikimbia haraka
kwenda kijiji.



Baada ya kutibu donda la
babake, babake aliweza
kusimama tena. Kijiji kizima
kilisherehekea na
kumpongeza Nangila.